# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA KWA WANAWAKE NA WATOTO -ZANZIBAR, MWAKA 2020

**Na: 13**

***Ofisi ya Takwimu Mkuu wa Serikali***

*Sanduku la barua: 2321, Zanzibar*
Simu +255242231869
Barua pepe:zanstat@ocgs.com
Tovuti: http://www.ocgs.go.tz

***Makao Makuu ya Polisi Zanzibar***

*Sanduku la barua:* 237, MMP Zanzibar
Faxi No: 0242231367
Barua pepe:cidhqznz@gmail.com

## Utangulizi

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kjinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6).

## Lengo

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera, na watoa maamuzi.

## Matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia

Jumla ya matukio 1,363 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwaka 2020.

Kulikuwa na waathirika 1,363 ambao waathirika Wanawake ni 217 (asilimia 15.9) na watoto ni 1146 sawa na asilimia 84.1, miongoni mwao wasichana ni 899 (asilimia 78.4) na wavulana ni 247 (asilimia 21.6).

Wilaya ya Mjini imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyegine (matukio 297), ikifuatia na wilaya ya Magharibi 'B' (matukio 273), na Wilaya ya Micheweni ina idadi ndogo zaidi ya matukio kuliko zote (matukio 41) (Kama inavyoonesha Jadweli nambari 1.1, 1.2 na 1.3).

Mlinganisho wa idadi ya matukio kwa mwaka uliopita imepungua kidogo kwa asilimia 0.4 kutoka matukio 1,369 kwa mwaka 2019 hadi 1,363 mwaka 2020 (Kama inavyoonesha Jadweli namba 1.2).


Miongoni mwa waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia waliobakwa ni 571, wanawake walikuwa 64 na wasichana ni 507, waliolawitiwa ni 102, kuingiliwa kinyume na maumbile ni 46 ambao mwanamke ni mmoja (1) na msichana 45. Kutorosha walikuwa ni 150 ,wanawake ni tisa (9),wasichana ni 139 na wavulana ni wawili (2), shambulio la aibu ni 74 ,wanawake ni 16, wasichana ni 50 na wavulana ni nane (8) na shambulio walikuwa 420 (wanawake ni 217, wasichana ni 158 na wavulana ni 135 (Kama inavyoonesha Kielelezo namba 1.2).

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio 681 sawa asilimia 59.4 ya matukio yote ya watoto ni zaidi ya robo mbili (2) ukilinganisha miaka mengine ya watoto . Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika wenye umri wa miaka 15-17 kwa mwezi uliopita imeongezeka kwa asilimia 9.7 kutoka matukio 621 kwa mwaka 2019 hadi matukio 681 kwa mwaka 2020. (Kama inavyoonesha Jadweli namba 1.5 na 1.6).

Matukio mengi yanaonesha yametokea majumbani ni matukio 1,270 sawa na asilimia 93.2 ikifuatiwa na sehemu nyengine (matukio 87) sawa na asilimia 6.4 na matukio yalobakia yametokea kazini na skuli / madrasa ni matukio matatu (3) sawa na asilimia 0.2 kwa kila eneo (Kama inavyoonesha Kielelezo namba 1.3).


Matukio 554 yapo mahakamani, matukio 382 yapo chini ya upelelezi wa Polisi, matukio 197 yapo kwa Muendesha Mashtaka, matukio 110 yamefungwa na Polisi, matukio 65 yametiwa hatiani, matukio 25 yamefungwa Mahakamani, matukio 18 hati ya Mashtaka, matukio 7 yameachiwa huru na matukio 5 yapo hatua DNA. (Kama inavyoonesha Jadweli namba 1.8)

**Kielelezo 1.1: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto kwa Wilaya, Mwaka , 2020**





**Chanzo: Makao** makuu ya Polisi –Zanzibar

**Kielelezo 1.2: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto, Mwaka 2020**





**Chanzo: Makao** makuu ya Polisi –Zanzibar.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Sehemu Yaliyotokea, Mwaka 2020**




Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Kielelezo 1.4: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia, Mwaka 2020**




Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 1.1: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mwaka 2020**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 60 | 44 | 2 | 1 | 3 | 5 | 5 |
| Kaskazini 'B' | 73 | 44 | 7 | 3 | 4 | 6 | 9 |
| Kati | 97 | 45 | 8 | 5 | 30 | 5 | 4 |
| Kusini | 51 | 32 | 2 | 1 | 7 | 4 | 5 |
| Mjini | 297 | 97 | 28 | 9 | 23 | 7 | 133 |
| Magharibi 'A' | 199 | 92 | 25 | 13 | 5 | 6 | 58 |
| Magharibi 'B' | 273 | 69 | 9 | 9 | 23 | 8 | 155 |
| Wete | 80 | 45 | 10 | 2 | 13 | 8 | 2 |
| Micheweni | 41 | 21 | 4 | 0 | 5 | 5 | 6 |
| Chake Chake | 115 | 56 | 5 | 1 | 25 | 7 | 21 |
| Mkoani | 77 | 26 | 2 | 2 | 12 | 13 | 22 |
| **Jumla** | **1363** | **571** | **102** | **46** | **150** | **74** | **420** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mwaka 2019 na Mwaka 2020**

| Wilaya | Idadi ya matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 |
| Kaskazini 'A' | 63 | 60 | 49 | 44 | 6 | 2 | 0 | 1 | 4 | 3 | 2 | 5 | 2 | 5 |
| Kaskazini 'B' | 83 | 73 | 53 | 44 | 6 | 7 | 0 | 3 | 9 | 4 | 11 | 6 | 4 | 9 |
| Kati | 101 | 97 | 49 | 45 | 13 | 8 | 2 | 5 | 27 | 30 | 10 | 5 | 0 | 4 |
| Kusini | 29 | 51 | 16 | 32 | 1 | 2 | 0 | 1 | 11 | 7 | 1 | 4 | 0 | 5 |
| Mjini | 267 | 297 | 99 | 97 | 31 | 28 | 1 | 9 | 6 | 23 | 11 | 7 | 119 | 133 |
| Magharibi 'A' | 285 | 199 | 135 | 92 | 50 | 25 | 1 | 13 | 30 | 5 | 19 | 6 | 50 | 58 |
| Magharibi 'B' | 235 | 273 | 90 | 69 | 27 | 9 | 1 | 9 | 22 | 23 | 11 | 8 | 84 | 155 |
| Wete | 95 | 80 | 42 | 45 | 6 | 10 | 2 | 2 | 32 | 13 | 7 | 8 | 6 | 2 |
| Micheweni | 64 | 41 | 38 | 21 | 2 | 4 | 0 | 0 | 12 | 5 | 8 | 5 | 4 | 6 |
| Chake | 102 | 115 | 53 | 56 | 9 | 5 | 0 | 1 | 19 | 25 | 21 | 7 | 0 | 21 |
| Mkoani | 45 | 77 | 27 | 26 | 6 | 2 | 1 | 2 | 8 | 12 | 3 | 13 | 0 | 22 |
| **Jumla** | **1,369** | **1,363** | **651** | **571** | **157** | **102** | **8** | **46** | **180** | **150** | **104** | **74** | **269** | **420** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 1.3: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya, Mwaka 2020**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 11 | 8 | 0 | 0 | 1 | 2 |
| Kaskazini 'B' | 13 | 7 | 0 | 2 | 1 | 3 |
| Kati | 9 | 6 | 1 | 1 | 1 | 0 |
| Kusini | 6 | 5 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini | 61 | 13 | 0 | 1 | 2 | 45 |
| Magharibi 'A' | 29 | 8 | 0 | 0 | 0 | 21 |
| Magharibi 'B' | 63 | 7 | 0 | 0 | 3 | 53 |
| Wete | 6 | 3 | 0 | 1 | 2 | 0 |
| Micheweni | 2 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 |
| Chakechake | 7 | 2 | 0 | 0 | 3 | 2 |
| Mkoani | 10 | 5 | 0 | 2 | 2 | 1 |
| **Jumla** | **217** | **64** | **1** | **9** | **16** | **127** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 1.4: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwaka 2020**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile - kike | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 49 | 36 | 2 | 1 | 3 | 0 | 1 | 3 | 3 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 60 | 37 | 7 | 3 | 2 | 0 | 4 | 1 | 4 | 2 |
| Kati | 88 | 39 | 8 | 4 | 29 | 0 | 3 | 1 | 3 | 1 |
| Kusini | 45 | 27 | 2 | 1 | 6 | 0 | 3 | 1 | 4 | 1 |
| Mjini | 236 | 84 | 28 | 9 | 22 | 0 | 5 | 0 | 36 | 52 |
| Magharibi 'A' | 170 | 84 | 25 | 13 | 5 | 0 | 6 | 0 | 17 | 20 |
| Magharibi 'B' | 210 | 62 | 9 | 9 | 23 | 0 | 5 | 0 | 51 | 51 |
| Wete | 74 | 42 | 10 | 2 | 11 | 1 | 6 | 0 | 2 | 0 |
| Micheweni | 39 | 21 | 4 | 0 | 4 | 0 | 4 | 0 | 4 | 2 |
| Chake Chake | 108 | 54 | 5 | 1 | 24 | 1 | 3 | 1 | 17 | 2 |
| Mkoani | 67 | 21 | 2 | 2 | 10 | 0 | 10 | 1 | 17 | 4 |
| **Jumla** | **1146** | **507** | **102** | **45** | **139** | **2** | **50** | **8** | **158** | **135** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 1.5: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwaka 2020**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana |
| 0-5 | | 11 | 10 | | | 2 | 0 | 0 | 3 | 7 | 7 | 5 |
| 6-10 | | 32 | 30 | | | 11 | 2 | 2 | 1 | 17 | 15 | 22 |
| 11-14 | | 117 | 35 | | | 21 | 0 | 23 | 1 | 9 | 38 | 44 |
| 15-17 | | 347 | 27 | | | 11 | 0 | 114 | 3 | 17 | 75 | 87 |
| **Jumla** | | 507 | 102 | | | 45 | 2 | 139 | **8** | **50** | **135** | **158** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 1.6: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwaka 2019 na Mwaka 2020**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 |
| 0-5 | 7 | 11 | 12 | 10 | 0 | 2 | 9 | 0 | 16 | 10 | 5 | 12 |
| 6-10 | 70 | 32 | 55 | 30 | 1 | 11 | 6 | 4 | 39 | 18 | 10 | 37 |
| 11-14 | 157 | 117 | 50 | 35 | 4 | 21 | 26 | 23 | 18 | 10 | 48 | 82 |
| 15-17 | 360 | 347 | 40 | 27 | 1 | 11 | 121 | 114 | 15 | 20 | 84 | 162 |
| **Jumla** | 594 | 507 | **157** | 102 | **6** | 45 | **162** | 141 | **88** | 58 | **147** | 293 |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi -Zanzibar

**Jadweli 1.7: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Maeneo yaliyofanyika Matukio, Mwaka 2020**

| Eneo la matukio | Kubaka | | | Kulawiti | | | Kuingilia kinyume na maumbile | | | Kutorosha | | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | | Shambulio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla |
| Nyumbani | 518 | [redacted] | 518 | [redacted] | 100 | 100 | 45 | [redacted] | 45 | 124 | 1 | 125 | 62 | 4 | 66 | 283 | 133 | 416 |
| Kazini | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 1 | 0 | 1 |
| Skuli/Madrasa | 1 | [redacted] | 1 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| Sehemu nyengine | 52 | [redacted] | 52 | [redacted] | 2 | 2 | 1 | [redacted] | 1 | 24 | 1 | 25 | 3 | 3 | 6 | 1 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **571** | [redacted] | **571** | [redacted] | **102** | **102** | **46** | [redacted] | **46** | **148** | **2** | **150** | **66** | **8** | **74** | **285** | **135** | **420** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 1.8: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Hatua Zilizochukuliwa, Mwaka 2020**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | Waathirika | | | Hatua zilizochukuliwa | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Wanawake | Watoto | | | | | | | | | | |
| | | | Wasichana | Wavulana | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwa huru | Zilizofungwa Polisi | DNA | Zilizopelekwa kwa Ofisi ya M'mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi wa Polisi | Hati ya Mashtaka | Kufungwa Mahakamani |
| Kubaka | 571 | 64 | 507 | | 187 | 44 | 4 | 5 | 38 | 92 | 175 | 10 | 16 |
| Kulawiti | 102 | | | 102 | 34 | 11 | 1 | 0 | 5 | 11 | 37 | 2 | 1 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 46 | 1 | 45 | | 23 | 0 | 0 | 0 | 1 | 4 | 17 | 1 | 0 |
| Kutorosha | 150 | 9 | 139 | 2 | 52 | 4 | 2 | 0 | 20 | 6 | 56 | 5 | 5 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 74 | 16 | 50 | 8 | 31 | 1 | 0 | 0 | 7 | 2 | 30 | 0 | 3 |
| Shambulio | 420 | 127 | 158 | 135 | 227 | 5 | 0 | 0 | 39 | 82 | 67 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **1,363** | **217** | **899** | **247** | **554** | **65** | **7** | **5** | **110** | **197** | **382** | **18** | **25** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi -Zanzibar

**Jadweli 1.9: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto, Mwaka 2019 na Mwaka 2020**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | |
| | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 | Mwaka 2019 | Mwaka 2020 |
| Kubaka | 651 | 571 | 57 | 64 | 594 | 507 | | |
| Kulawiti | 157 | 102 | | | | | 157 | 102 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 8 | 46 | 2 | 1 | 6 | 45 | | |
| Kutorosha | 180 | 150 | 18 | 9 | 161 | 139 | 1 | 2 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 104 | 74 | 16 | 16 | 81 | 50 | 7 | 8 |
| Shambulio | 269 | 420 | 122 | 127 | 65 | 158 | 82 | 135 |
| **Jumla** | **1,369** | **1,363** | **215** | **217** | **907** | **899** | **247** | **247** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi -Zanzibar

**Zingatia Maelezo**

**Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia**

Kitendo chochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi au ya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wa ngono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile na shambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hii ya mwaka 2004. Sheria hii imetungwa pamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenye shehemu ya kumi na tatu (Section thirteen) ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyo haviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadi kifungo cha maisha.

**Kwa ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na:**

***Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali***
***Sanduku la barua, 2321***
***Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz***

***Makao Makuu ya Polisi Zanzibar***
***Sanduku la barua, 237, MMP, Zanzibar***
***Barua pepe:cidphqznz@gmail.com***